**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

# 04 HISABATI

**Muda: Saa 1: 30** **Mwaka: 2018.**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**
3. Kila swali lina **alama (10)**

| **Na.** | | **Swali** | **Nafasi ya Kazi** | **Jibu** |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | (a) | Andika namba 20,392 kwa maneno. | | |
| | (b) | Andika XXXIV kwa namba za Kiarabu. | | |
| | (c) | Andika thamani ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba 3$\underline{4}$02. | | |
| | (d) | Andika namba ifuatayo kwa kirefu: 9536 | | |
| | (e) | Wanafunzi walipanda miti 680 ili kulinda mazingira ya shule.Andika idadi ya miti iliyopandwa kwa maneno. | | |
| **2.** | (a) | Jaza namba inayofuata katika mpangilio wa namba zifuatazo:1, 3, 5, 7, ______. | | |
| | (b) | Panga namba zifuatazo kwa mpangilio unaoanza na namba ndogo hadi namba kubwa zaidi: 20, 4, 12, 7, 16, 3, 10. | | |
| | (c) | Andika namba inayokosekana ili kukamilisha mpangilio wa namba za Kirumi ufuatao: XXII, XXV, XXVIII, _, XXXIV. | | |
| | (d) | Andika namba inayokosekana katika mfululizo ufuatao: 36, 33, 30, ___, 24. | | |




Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Nafasi ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | (e) | Chura aliruka hatua tatu zenye urefu sawa hadi kufikia m 21. Ikiwa aliruka hatua ya nne yenye urefu sawa na hatua za mwanzo, je, alifikia umbali gani? | | |
| **3.** | (a) | Jumlisha; 1715 + 263 = | | |
| | (b) | Gawanya;<br>20 ) 600 | | |
| | (c) | Shule ya msingi Mkombozi ina wanafunzi 826. Ikiwa idadi ya wavulana ni 408, je, wasichana ni wangapi?. | | |
| | (d) | Zidisha; 49 x 53 = | | |
| | (e) | Kijo alikuwa na shilingi 9,750. Alimpa rafiki yake kiasi Fulani cha fedha na kubakiwa na shilingi 3,250. Je, alimpa rafiki yake shilingi ngapi? | | |
| **4.** | (a) | Andika jina la umbo lifuatalo ambalo urefu wa pande zake zote nne zinalingana:<br> | | |
| | (b) | Sehemu zilizogawanywa katika umbo lifuatalo zinalingana.<br>Andika sehemu iliyowekwa kivuli.<br> | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Nafasi ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | (c) | Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo:<br><br> | | |
| | (d) | Mzingo wa pembetatu ni sm 48. Ikiwa urefu wa upande wa kwanza ni sm 12 na urefu wa upande wa pili ni sm 20,<br>tafuta urefu wa upande wa tatu. | | |
| | (e) | Mstatili una mzingo wa sm 80 na urefu wa sm 25. Tafuta upana wake. | | |
| **5.** | (a) | Jumlisha; Sh. 1940 + sh. 265= | | |
| | (b) | Toa; Sh. 3150 - sh. 1500= | | |
| | (c) | Zidisha;<br>Sh 3 0 0<br>× 2 5<br>______ | | |
| | (d) | Mariamu alikuwa na shilingi 8,650. Baadaye, alitumia shilingi<br>3,800. Je, alibakiwa na shilingi ngapi? | | |
| | (e) | Noti ya Tanzania ya shilingi 10,000 ina noti ngapi zenye thamani ya shilingi 1,000? | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org